

Ikiwa utaiamini injili hii ya Yesu Kristo, kwani imani kama ya mtoto mpokee Yesu kwa kuliitia jina lake. Tafadhali fanya hivyo sasa kama kungali na mwaliko wa wokovu. Yohana Mtakatifu 3:36 *“Amwaminiye Mwana yuna uzima wa milele; asiye mwamini Mwana hataona uzima, bali ghadhabu ya Mungu inamkalia.”* Ufunuo wa Yohana 20:15 *“Na iwapo mtu yeyote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto.”*



P.O. BOX 1115 • YORK, SC 29745 • 803-684-1535  
WWW.HOPETRACTS.ORG  
Are You 100% Sure? (Swahili) Tract 506



Biblia ni **neneo la Mungu**.

**Mungu asema** sote tuna mwaliko wa kukutana naye tukifa. Waraka kwa Wahebrania 9:27: *“Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja, na baada ya kufa hukumu;”* Jambo la muhimu zaidi maishani ambalo waweza kufanya ni kujtayarisha kukutana na Mungu. Je, mtu aweza kuwa na uhakika bila tashwishi yoyote kwamab ataenda mbinguni?

**Mungu asema** unaweza kujua! Waraka wa Yohana wa kwanza 5:13: *“Nimewaandikia ninyi mabo hayo, ili mjue kuwa mna uzima wa milele, ninyi mnaoliamini Jina la Mwana wa Mungu.”* Watu wengi hudhani kwamba utu wema utawapeleka mbinguni.

**Mungu asema** hakuna aliye mwema. Warumi 3:10,12b,23 *“Kama ilivyoandikwa, ya kwamba, Hakuna mwenye haki hata mmoja...Hakuna mtenda mema, la! Hata mmoja...Kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu;”*

**Mungu asema** kuna deni la dhambi ambalo lazima lilipwe. Warumi 6:23a *“Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti...”* Yesu alitufia ili tusiende jehanamu. Yohana Mtakatifu 3:16 *“Kwa maana jinsi Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanawe wa pekee, ili kila mti amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.”*

Warumi 5:8 *“Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipoku tungali wenye dhambi.”* Yesu alimwaga damu yake ya thamana kusafisha dhambi zetu. Wakolosai 1:14 *“ambaye katika yeye tuna ukombozi, yaani, msamaha wa dhambi.”* Siku tatu baada ya kuzikwa Yesu alifufuka kutoka katika wafu.

**Mungu asema** lazima tuliadini jambo hili si kwa akili tu bali kwa moyo wetu wote. Warumi 10:9 *“Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka.”*

**Mungu asema** lazima utubu. Luka Mtakatifu 13:3 *“Nawaambia, Sivyoy; lakini msipotubu, ninyi nyote mtaangamia vivyo hivyo.”* Hii yamaanisha kukiri dhambi zako, kutoka katika dhambi na kumgeukia Yesu na kumpokea kuwa Bwana na Mwokozi wako. 2 Wakorintho 7:10 *“Maana huzuni iliyo kwa jinsi ya Mungu hufanya toba liletalo wokovu lisilo na majuto...”* Yohana Mtakatifu 1:12 *“Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake.”*

**Mungu asema** yeyote aweza kuokoka. Warumi 10:13 *“Kwa kuwa, Kila atakayeliita Jina la Bwana ataokoka.”*